



UPATIKANAJI WA IDARA YA VERMONT HEALTH

**Mwongozo wa
Mipango ya Huduma ya Afya**



Jedwali la Yaliyomo

Jedwali la Yaliyomo	2
Karibu kwenye Mpango wako wa Green Mountain Care	4
Majina ya Mpango.....	4
Kadi yako ya Green Mountain Care	4
Udanganyifu, Uharibifu na Matumizi Mabaya	4
Huduma ya Afya na Rufaa	5
Mtoa Huduma ya Msingi (PCP)	5
Utunzaji wa Baada ya Kazi	5
Wataalamu.....	6
Ikiwa Daktari Wako Hakubali Green Mountain Care.....	6
Ukaguzi wa Mara kwa Mara	7
Medicaid na Dkt. Dynasaur	7
Huduma Zinzolipiwa na Bima Yako (Huduma Unazoweza Kupata).....	7
Malipo Nyongeza ya Medicaid.....	8
Malipo ya Bima.....	8
EPSDT ni nini?	8
Huduma Zisizolipiwa na Bima Yako.....	9
Kupata Huduma Zinzolipiwa katika Mipango ya Medicaid na Dkt.Dynasaur	9
Vighairi	9
Idhini ya Awali	10
Vifaa vya Kudumu vya Matibabu (DME).....	10
Dawa na Idhini ya Awali.....	11
Dharura	12
Unapolazimika Kulipa	12
Ukipokea Bili.....	13
Ikiwa Una Bima Nyingine.....	13
Haki na Majukumu Yako	13
Una haki ya	13
Utashi wa Kuishi na Maelekezo ya Mapema.....	14
Kuchanga Viungo.....	15
Kushiriki Taarifa na Mtoa Huduma wako wa Msingi (PCP).....	15
Notisi ya Kanuni za Faragha.....	16
Mpango wa Uhakikisho wa Ubora	16
Hatua ya Kuchukua Usipokubaliana na Uamuzi Tuliofanya	17
Hatua ya Kwanza ni Kuomba Rufaa ya Ndani.....	18
Aina nyingine za malalamiko kuhusu huduma zako za afya – unaweza kuwasilisha Nung’uniko ...	21

Unahitaji Usaidizi?	22
Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain	22
Ofisi ya Wakili wa Huduma ya Afya (HCA).....	22
Maelezo ya Ziada	22
Mipango Mingine.....	22
Huduma za Utunzaji wa Watu Wazima	22
Mpango wa Huduma za Wasaidizi.....	23
Huduma Jumuishi za Watoto (CIS).....	23
Huduma Jumuishi za Watoto - Uingiliaji Kati wa Mapema (CIS-EI).....	23
Huduma za Utunzaji Binafsi wa Watoto.....	23
Kliniki za Watoto wenye Mahitaji Maalum ya Kiafya (CSHN).....	23
Machagu ya Utunzaji.....	23
Huduma za Ulemavu wa Kiukuaji	24
Mpango wa Usaidizi wa Kifedha.....	24
Ufadhili Rahisi wa Familia.....	24
Huduma ya Uuguzi Unaotumia Teknolojia ya Hali ya Juu	24
Huduma za Utunzaji wa Nyumbani.....	25
Kliniki Maalum.....	25
Huduma Maalum.....	25
Mpango wa Vermont wa Kugundua na Kutibu Mapema Matatizo ya Masikio	25
Afya ya Akili.....	25
Huduma za Watu Wazima Wasioishi Kituoni	26
Huduma kwa Watoto, Vijana na Familia	26
Urekebishaji na Matibabu ya Kijamii.....	26
Huduma za Dharura.....	26
Mpango wa Majeraha ya Ubongo	26
Mpango kwa Wanawake, Watoto Wachanga na Watoto Wakubwa (WIC).....	26
Makinika! Ikiwa unahitaji usaidizi katika lugha yako, tafadhali piga simu kwa 1-800-250-8427	27

Oktoba 2023



Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain

Maswali: Piga simu 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898

Unaweza pia kupata huduma za wakalimani na miundo mbadala bila malipo.

Karibu kwenye Mpango wako wa Green Mountain Care

Sehemu ya kwanza ya kitabu hiki ina taarifa ya jumla ya mpango ambayo inatumika kwa mipango yetu yote ya huduma ya afya. Sehemu za baadaye zinatoa maelezo kuhusu mpango ambao umejiunga nao.

Ikiwa hujui ni mpango gani uliojiunga nao, au ikiwa una maswali yoyote, kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja cha Vermont Health Connect na Green Mountain Care kupitia 1-800-250-8427. Piga simu Jumatatu hadi Ijumaa, 8:00 a.m. hadi 4:30 p.m. (hufungwa wakati wa sikukuu). Nambari hii pia inaweza kupatikana kwenye sehemu ya nyuma ya kadi yako ya Green Mountain Care.

Green Mountain Care inahimiza watoa huduma kutoa huduma bora, zinazohitajika kiafya kwa washiriki wote, na haiwahimizi madaktari kupunguza, kukataa au kuzuia huduma zinazohitajika kiafya. Green Mountain Care haitakubagua kwa msingi wa hali zilizopigwa marufuku na shirikisho. Maelezo zaidi kuhusu Mipango ya Green Mountain Care yanapatikana kwa kukipigia simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwenye 1-800-250-8427.

Ikiwa ungependa kughairi bima yako ya Green Mountain Care, kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja cha Vermont Health Connect na Green Mountain Care kupitia 1-800-250-8427. Ili kughairi bima yako kwa maandishi, tafadhali tuma ombi lako kwa:

DCF/Idara ya Huduma za Uchumi
ADPC
103 South Main Street
Waterbury, VT 05671-1500

Majina ya Mpango

Medicaid ni mpango wa huduma ya afya kwa watoto, wazazi, watunzaji, wazee, watu wenye ulemavu wanaotimiza miongozo ya mpango, na watu wazima fulani wasio na watoto wanaokidhi vigezo fulani ya ustahiki. Medicaid ya huduma ya muda mrefu inapatikana kwa watu wanaokidhi vigezo vya matibabu (kama ilivyobainishwa na Idara ya Watu wenye Ulemavu, Wazee na Wanaoishi Maisha ya Kujitegemea) na miongozo ya mapato na rasilimali.

Dr. Dynasaur hutoa bima ya Medicaid isiyolipishwa au ya bei nafuu kwa watoto, vijana wa umri wa chini ya miaka 19, na wanawake wajawazito.

Kadi yako ya Green Mountain Care

Kadi yako ya Kitambulisho chako itatumwa nyumbani kwako. Tafadhali waonyesha wahudumu kadi hii unapoenda kupaokea huduma ya afya. Usipopata kadi yako mpya ya kitambulisho ndani ya mwezi mmoja baada ya kupata kitabu hiki cha mwongozo, au ukipoteza kadi yako, kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427 na uombe kadi mpya. Ikiwa una bima nyingine ya huduma ya afya, onyesha mtoa huduma wako kadi zako zote mbili za kitambulisho cha bima.

Udanganyifu, Uharibifu na Matumizi Mabaya

Kitengo Maalum cha Uchunguzi (SIU) kinafanya kazi ya kuanzisha na kudumisha uadilifu ndani ya Mpango wa Medicaid na kushiriki katika shughuli za kuzuia, kugundua na



kuchunguza matukio ya udanganyifu, uharibifu na matumizi mabaya ya watoaji na wapokeaji wa Medicaid. SIU inahakikisha pesa za walipa kodi zinatumiwa ipasavyo kwa ajili ya afya na ustawi wa wapokeaji wanaohitaji.

Ikiwa unashuku mtoa huduma wa Medicaid au mpokeaji wa Medicaid amehusika katika ulaghai, uharibifu au matumizi mabaya ya Mpango wa Medicaid, tafadhali ripoti wasiwasi wako kwa SIU kupitia mojawapo ya njia zilizo hapa chini:

Tovuti: <https://dvha.vermont.gov/>

Bofya: Ripoti Ulaghai, Uharibifu na Matumizi Mabaya ya Medicaid

Bofya: Fomu ya Rufaa ya Ulaghai na Matumizi Mabaya

Barua pepe: ReportMedicaidFraud@vermont.gov

Simu: 802-241-9210

Anwani ya Barua ya Posta:

Kitengo Maalum cha Uchunguzi cha DVHA

NOB 1 South, 280 State Drive

Waterbury, VT 05671-1010

Faksi: 802-871-3090 (faksi ya moja kwa moja kwa "Kitengo Maalum cha Uchunguzi cha DVHA")

Huduma ya Afya na Rufaa

Mtoa Huduma ya Msingi (PCP)

Neno “msingi” linamaanisha kwanza. PCP wako ndiye unayempigia simu kwanza unapohitaji huduma ya matibabu. PCP wako atatoa huduma yako ya afya na kushirikiana na wewe kupanga huduma maalum wakati unapoihitaji.

Ikiwa PCP wako ni mgeni kwako, omba PCP wako wa zamani atume rekodi zako za matibabu kwa PCP wako mpya. Piga simu kwa PCP wako mpya kusemaa kuwa rekodi zinakuja. Ni muhimu kwa PCP wako awe na rekodi zako za matibabu.

Utunzaji wa Baada ya Kazi

Jaribu kumwona PCP wako ukitaka kutibiwa baada saa za kawaida za kazi. Ikiwa una tatizo la kiafya la haraka wakati ofisi ya Mtoa Huduma ya Msingi (PCP) imefungwa, unaweza kupiga simu kwa ofisi ya PCP wako na uombe usaidizi au ushauri.

Ofisi ya PCP wako itakuwa na mtu anayepatikana saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki ili kukusaidia. Tafadhali angalia sehemu ya mwongozo huu yenye kichwa **Dharura** ili upate maelezo zaidi kuhusu huduma za dharura na haraka.



VERMONT

Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain

Maswali: Piga simu 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898

Unaweza pia kupata huduma za wakalimani na miundo mbadala bila malipo.

Wataalamu

Mtaalamu ni mtu ambaye amepewa mafunzo ya ziada na anafanya kazi kwa aina fulani ya matatizo ya huduma ya afya. Kwa mfano, ikiwa una tatizo la moyo, PCP wako atakusaidia kuweka miadi kwa mtaalamu wa moyo. Hatua hii inaitwa “rufaa.” Katika hali nyingi, lazima uone PCP wako kabla ya kwenda kwa mtaalamu. PCP wako anaweza kukusaidia kuamua ikiwa unahitaji mtaalamu na kukusaidia kuchagua mhudumu utakayemuona. Lazima upate rufaa kutoka kwa PCP wako kabla ya kwenda kwa mtaalamu ambaye si mtoa huduma wa Medicaid. Usipopata mwaliko kutoka kwa PCP wako kabla ya kwenda, huenda utazalima kulipia ziara hiyo.

Ikiwa Daktari Wako Hakubali Green Mountain Care

Ukiona mtoa huduma sasa ambaye hayupo kwenye mpango yako, unaweza kuendelea kwenda kwa mtoa huduma huyo kwa hadi siku 60 baada ya kujiunga na mpango. Huenda jambo hili likafanyika tu ikiwa:

- Una ugonjwa unaotishia maisha, **au**
- Una ugonjwa unaolemaza au kuzorotesha, **au**
- Una ujauzito wa zaidi ya miezi mitatu, **na**
- Mtoa huduma anakubali bei za mpango na kufuata sheria za mpango.

Ili kupanga nyongeza ya siku 60, au kupata maelezo zaidi kuhusu rufaa na watoa huduma katika mipango yetu, piga simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427.

Unaweza pia kuona ni watoa huduma gani wanaokubali huduma ya Green Mountain Care kwa kutembelea vtmedicaid.com, na kubofya kwenye Utafutaji wa Mtoa Huduma. Watoa huduma walioorodheshwa kama wa “nje ya mtandao” huenda wasikubali bima ya Green Mountain Care.

Mtoa huduma yeyote anayekuhudumia lazima akubali Green Mountain Care. Wasipofanya hivyo, hawatalipwa na Green Mountain Care kwa kukutibu na utatakiwa kulipia huduma hizo. Ikiwa una bima nyingine ya afya ambayo inaweza kulipia matibabu yote au sehemu yake, mtoa huduma wako lazima akubali mipango yote miwili ya bima ya afya.

Ikiwa Unahitaji Huduma Nje ya Mtandao wa Vermont Medicaid

Tuna mtandao mkubwa sana wa watoa huduma ikiwa ni pamoja na aina nyingi za wataalamu. Mtandao wetu umeundwa kushughulikia mahitaji mbalimbali ya matibabu. Katika hali chache, mtandao huu hauwezi kutibu matatizo fulani maalum ya huduma ya afya. Ikiwa unaamini unahitaji huduma maalumu ambayo huwezi kupata kutoka kwa mtoa huduma wa Vermont Medicaid, wasiliana na PCP wako ili kujadili mahitaji yako. PCP wako anaweza kukuomba ruhusa ya kupokea huduma kutoka kwa mtoa huduma ambaye si sehemu ya mtandao wetu ikiwa:

- Utunzaji unaohitaji ni wa lazima kiafya na unalipiwa na Vermont Medicaid
- Mtoa huduma unayetaka kuona anakubali kufuata masharti yetu
- Tunaweza kubaini kuwa huduma unayohitaji haipatikani kwenye mtandao wetu

Ukaguzi wa Mara kwa Mara

Daima ni bora kuzuia matatizo ya afya kabla yaanze. Njia moja ya kufanya hivyo ni kuwa na ukaguzi wa mara kwa mara kwa PCP wako. Daktari wako anaweza kukusaidia kuamua ni mara ngapi utafanyiwa uchunguzi. Muulize mtoa huduma wako wa msingi kuhusu uchunguzi maalum wa huduma za afya ambao unapaswa kuwa nao kulingana na umri wako na sababu za hatari za mtu binafsi.



Idara ya Afya ya Vermont hutoa ushauri kuhusu vipimo. Ili upate maelezo zaidi, piga simu kwa Idara ya Afya ya Vermont kwenye 1-800-464-4343, au utembelee tovuti kwenye www.healthvermont.gov.

Medicaid na Dkt. Dinosaur

Huduma Zinazolipiwa na Bima Yako (Huduma Unazoweza Kupata)

- Mipango mingi ya Green Mountain Care inagharimia mtoa huduma na ziara za wataalamu, huduma ya hospitali, dawa za kuagizwa na daktari, na huduma zingine nyingi zilizo na sheria na mipaka. Unapaswa kumwona mtoa huduma wako wa msingi kwanza kabla ya kufanya miadi ya huduma na mtaalamu. Mtoa huduma wako anapaswa kuwasiliana na Huduma za Mtoa Huduma ili kuhakikisha kuwa huduma inalipiwa na bima yako kabla ya kuitoa. Ikiwa una swali kuhusu huduma ambayo haijaorodheshwa, kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427. Utunzaji wa hospitali unaopata bila kulazwa hospitalini;
- Huduma za dharura;
- Kulazwa hospitalini (kama vile upasuaji unaokuhitaji kulazwa);
- Ujauzito, uzazi na utunzaji wa watoto wachanga (kabla na baada ya kuzaliwa);
- Huduma za afya ya akili na utumiaji wa dawa za kulevya, pamoja na matibabu ya afya ya akili (hii ni pamoja na ushauri nasaha na matibabu ya kisaikolojia);
- Dawa za kuagizwa na daktari;
- Huduma na vifaa vya ukarabati na makazi (huduma na vifaa vya kusaidia watu walio na majeraha, ulemavu, au hali sugu kupata au kurejesha ustadi wa kiakili na kimwili);
- Huduma za maabara;
- Huduma za kuzuia na ustawi, na udhibiti wa magonjwa sugu;
- Huduma za meno, macho na masikio;
- Huduma za matibabu ya watoto; na
- Usafiri kwa Matibabu Yasiyo ya Dharura.

Malipo Nyongeza ya Medicaid

- Washiriki wa Medicaid hulipa \$3 kwa kila ziara ya daktari wa meno.
- Wanachama wa Medicaid hulipa \$1, \$2 au \$3 kwa dawa zinazoagizwa na daktari.
- Wateja wa Medicaid hulipa \$3 kwa siku kwa kila hospitali kwa ziara za hospitali za wagonjwa wasiolazwa.

Baadhi ya huduma zinazotolewa katika ofisi nje ya hospitali ni huduma za hospitali za wagonjwa wasiolazwa. Muulize mtoa huduma wako ikiwa huduma itatozwa kama ziara ya hospitali ya wagonjwa wasiolazwa.

Ikiwa ni hivyo, malipo yako yatakuwa \$3.

Watoto wengi, wanawake wajawazito, na watu walio katika vituo vya wazee hawalazimiki kulipa malipo nyongeza. Watu waliojiandikisha katika Mipango ya Matibabu ya Saratani ya Matiti na Kizazi hawahitaji kulipa malipo nyongeza.

Hutakiwi kulipa malipo nyingeza kwa ajili ya:

- Huduma za kuinga
- Huduma za upangaji uzazi na vifaa
- Huduma za dharura
- Huduma zinazohusiana na unyanyasaji wa kingono

Malipo ya Bima

Baadhi ya washiriki wa Dr. Dynasaur wanaweza kuhitaji kulipa malipo ya kila mwezi. Kiasi cha bima cha familia hutegemea mapato ya familia, ukubwa na hali ya bima ya afya.

Unapopata bili yako ya kwanza, ni muhimu kulipa mara moja ili bima yako ianze kutumika. Endelea kulipa kwa wakati ili usipoteze bima yake. Ukipoteza bili yako ya malipo, kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja ili ujue ni kiasi gani unachodaiwa na jinsi ya kulipa.

EPSDT ni nini?

EPSDT ni Medicaid na Dr. Dynasaur kwa watoto na vijana chini ya umri wa miaka 21.

Inajaribu kudumisha afya bora zaidi kwa watoto. **EPSDT** inamaanisha “Early Periodic Screening Diagnostic Treatment” yaani Matibabuya Mapema ya Utambuzi na Uchunguzi wa Mara kwa Mara. Inapaswa:

- Kugundua matatizo mapema, kuanzia wakati wa kuzaliwa
- Kujumuisha ziara za daktari za kufanya vipimo kila mara
- Kutumia vipimo vya ukaguzi ili kugundua matatizo yoyote
- Kufanya vipimo vya ufuatiliaji ikiwa matatizo yanapatikana na
- Kutibu matatizo yoyote ya kiafya yanayopatikana

Utaratibu wa EPSDT

EPSDT ipo katika sheria ya shirikisho. Inaliagiza Jimbo kulipia huduma yoyote ya afya inayohitajika. **Huduma inayohitajika kimatibabu** inamaanisha ni kwa tatizo hilo la kiafya **na** kwamba hivyo ndivyo madaktari wengi wangepanya kutibu taizo hilo. Inalipia huduma zaidi kuliko bima ya Medicaid kwa watu wazima. Baadhi ya huduma zinahitaji kuthibitishwa kwanza kupitia mchakato wa idhini ya awali.

Huduma za Bima za EPSDT

- Uchunguzi wa mara kwa mara
- Vipimo vya jinsi mtoto anavyokua na kujifunza
- Chanjo
- Vipimo vya macho
- Vipimo vya kusikia
- Vipimo vya sumu ya madini ya risasi
- Matibabu ya meno
- Ushauri nasaha

Je, mtoto hupimwa mara ngapi?

Kuna orodha ya [vipimo vya afya ambavyo](#) watoto na vijana wanapaswa kupata kila mwaka. Pia kuna orodha [tofauti ya vipimo vya meno](#).

EPSDT hailipii:

- Huduma au vitu ambavyo haviko katika sheria za shirikisho za Medicaid (Sehemu ya 1905(a) ya Sheria ya Bima ya Jamii).
- Huduma ya majaribio ambayo sio salama au haifanyi kazi.
- Huduma au bidhaa za bei ghali ikiwa mojawapo ya bei nafuu itafanya kazi sawa.
- Huduma ambazo si za kimatibabu.

Ili upate maelezo zaidi, tembelea www.dvha.vermont.gov/members au upige simu 1-800-250-8427.

Huduma Zisizolipiwa na Bima Yako

- Majeraha yanayohusiana na kazi ambayo yanapaswa kulipwa na Fidia ya Mfanyakazi,
- Gharama za huduma zilizoagizwa na mahakama isipokuwa pia ni muhimu kiafya,
- Huduma za majaribio au uchunguzi,
- Huduma za urembo (huduma za kuboresha jinsi unavyoonekana),
- Huduma ambazo si muhimu kimatibabu,
- Tiba ya chunusi, tiba ya kupapaswa au ukandaji,
- Matibabu ya uzazi (huduma zinazokusaidia kupata ujauzito),
- Uanachama wa klabu za afya, na
- Huduma katika nchi za nje.

Kupata Huduma Zinazolipiwa katika Mipango ya Medicaid na Dkt.Dynasaur

Vighairi

Wakati huduma hailipiwi na Medicaid kwa watu wazima wenye umri wa miaka 21 na zaidi, unaweza kuomba huduma ilipiwe na bima kwa ajili yako. Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kinaweza kukusaidia kuwasilisha ombi hili. Wewe na mtoa huduma wako mtaombwa kutoa



VERMONT

Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain

Maswali: Piga simu 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898

Unaweza pia kupata huduma za wakalimani na miundo mbadala bila malipo.

taarifa kwa Idara ya Vermont Health Access kuhusu huduma na kwa nini unaihitaji. Tutakutumia jibu kwa njia ya barua baada ya siku 30 hivi. Huduma zote muhimu za matibabu zinalipiwa na EPSDT kwa mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 21. Ikiwa huduma haijaorodheshwa kama inayolipiwa na bima, mtoa huduma wako lazima aombe ithibitishwe kwa idhini ya awali.

Ili upate maelezo zaidi kuhusu mchakato huu, au uombe kighairi, kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kupitia 1-800-250-8427. Fomu hizi pia zinaweza kupatikana mtandaoni kwenye www.dvha.vermont.gov/members/vermont-medicaid-programs/member-information/coverage-exceptions

Idhini ya Awali

Green Mountain Care inashirikiana na madaktari, wauguzi na wataalamu wengine ili kuhakikisha kuwa huduma za afya unazopata ni muhimu kimatibabu. Baadhi ya huduma na dawa zinahitaji kuidhinishwa kabla ya kuzipata. Hatua hii inaitwa idhini ya awali. Watoa huduma wako wanajua huduma na dawa hizo ni nini, na wataomba idhini ya mapema kwa ajili yako.

Maamuzi kuhusu idhini ya awali yanafanywa ndani ya siku tatu ikiwa hati zote zinazohitajika zimepokelewa kwa ajili ya ukaguzi. Wewe na mtoa huduma wako mtapata barua inayokufahamisha kuhusu uamuzi huo. Idhini ya awali haihitajiki kwa huduma za dharura.

Vifaa vya Kudumu vya Matibabu (DME)

Vifaa vya Kudumu vya Matibabu (DME) ni kitu ambacho unaweza kutumia kusaidia kurahisisha maisha na hali yako ya matibabu. Viti vya magurudumu na vitanda vya hospitali ni mifano ya DME.

Nina Medicaid na ninahitaji DME. Ninaweza kuipataje?

1. Mtoa huduma wako atakuelekeza kwa mkaguzi kwa ajili ya tathmini.

- Watathmini wengi ni wataalamu wa kimwili au wa shughuli za maisha. Mtathmini atanzisha mchakato wa kukutathmini. Huenda ukalazimika kusubiri tathmini ikiwa mtathmini ana shughuli nyingi. Unaweza pia kusubiri ikiwa muuzaji wa DME anahitaji kukusaidia kujaribu vifaa. Muuzaji wa DME ni kampuni inayotoa vifaa.
- *Kumbuka:* Ikiwa DME unayohitaji ni rahisi, huenda usihitaji tathmini. Ikiwa mtoa huduma wako anasema huhitaji tathmini, ruka hadi hatua ya 2.
- Mtathmini ataamua ni aina gani ya DME unayohitaji na atume fomu ya tathmini kwa mtoa huduma wako.

2. Mtoa huduma wako ataandika agizo la daktari.

- Mtoa huduma wako atatia saina fomu ya tathmini na kutuma maagizo ya dawa ya DME kwa muuzaji.

3. Muuzaji wa DME ataomba Medicaid idhini ya awali.

Ikina huhitaji idhini ya awali, ruka hadi hatua ya 5.



- Ikiwa unahitaji idhini ya awali ya DME, muuzaji atatuma taarifa kukuhusu wewe na DME unayohitaji kwa Medicaid. Idhini ya awali inamaanisha kuwa Medicaid inapaswa kuthibitisha kabla ya kupokea vifaa.
- Mkaguzi wa kimatibabu atakagua maelezo yako. Mkaguzi ataamua ikiwa una hitaji la matibabu la vifaa.
- Mkaguzi wa kimatibabu anaweza kuhitaji taarifa zaidi ili kuamua ikiwa una hitaji la matibabu la vifaa hivyo. Ikiwa mkaguzi anahitaji taarifa zaidi, Medicaid itamwomba muuzaji wa DME kuituma. Muuzaji lazima atume taarifa ndani ya siku 12. Baada ya Medicaid kupata taarifa zote, mkaguzi lazima afanye uamuzi ndani ya saa 72.
- Ikiwa DME ni sehemu ya ziara ya Afya ya Nyumbani utahitaji kutembelewa na mtoa huduma wako, mara ya kwanza DME itaagizwa

4. Medicaid itakutumia Ilani ya Uamuzi

- Medicaid itakuarifu uamuzi huo kwa kukutumia barua inayoitwa Ilani ya Uamuzi. Medicaid pia itatuma barua kwa mtoa huduma wako na muuzaji wa DME. Katika jimbo la Vermont, Idara ya Vermont Health Access (DVHA) inaendesha Medicaid, kwa hivyo barua zitatoka kwa DVHA.

5. Muuzaji wa DME atakupatia DME.

Ikiwa Medicaid itaidhinisha, muuzaji wa DME atakupatia DME au kuagiza kwa niaba yako.

Ikiwa Medicaid haiidhinishi, unaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo. Ili uombe rufaa, kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427. Medicaid imefanya juhudi kufupisha muda ambao inachukua kuidhinisha ombi la DME huko Vermont. Kwa viti tata vya magurudumu, inachukua takriban siku 9. Kipindi hiki ni kifupi kuliko muda ambao sheria za Medicaid zinahitaji. Pia ni kifupi kuliko wastani wa kitaifa. Kwa vifaa rahisi, kipindi hiki huwa kifupi. Ikiwa una Medicaid na Medicare au mpango mwingine wa bima, mchakato huu unaweza kuchukua muda mrefu.

Dawa na Idhini ya Awali

Green Mountain Care, kama kampuni nyingine za bima, inafanya kazi ya kutoa bima bora ya afya kwa gharama nafuu. Ili kusaidia kupunguza gharama, Green Mountain Care inawaomba watoa huduma kuagiza dawa kutoka kwenye orodha ya dawa zinazopendelewa. Baadhi ya dawa kwenye Orodha ya Dawa Zinazopendelewa ni dawa za kawaida za bei nafuu. Zinafanya kazi sawa na dawa za bei ghali zinazotangazwa na makampuni ya dawa. Watoa huduma wanapaswa kuagiza na wafamasia lazima wajaze dawa inayolingana na bei ya chini kabisa ambayo inafaa kitabibu. Ukikataa ubadilishanaji huu, mpango wako wa Green Mountain Care huenda usishughulikie dawa isiyopendekezwa.

Lazima upewe dawa za matibabu fulani ya muda mrefu kwa mgao wa siku 90. Hizi ni dawa zinazotumiwa mara kwa mara ili kudhibiti matatizo maalum ya kiafya. Zinategemea hali ya mtu na zinajumuisha, lakini si tu, dawa za kudhibiti shinikizo la damu, mafuta ya moyo na kisukari. Mara ya kwanza unapojaribu dawa, inaweza kuwa kwa muda mfupi wakati wewe na mtoa huduma wako mtaamua kama inakufaa. Baada ya hapo, utapata mgao wa siku 90.



VERMONT

Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain

Maswali: Piga simu 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898

Unaweza pia kupata huduma za wakalimani na miundo mbadala bila malipo.

Ikiwa mtoa huduma wako anaamini unahitaji dawa ambayo haipendelewi au haipaswi kuwa kwa mgao wa siku 90, anaweza kuomba idhini yetu kulipia dawa hiyo. Ikiwa ungependa kupata nakala ya orodha ya dawa unazopendelea au orodha ya dawa zinazohitaji usambazaji wa siku 90, kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja au angalia [orodha ya dawa unazopendelea](#) mtandaoni.

Dharura

Hali ya dharura ni ugonjwa wa ghafla na usiotarajiwa, hali ya matibabu, au hali ya afya ya akili, na dalili ambazo unaamini zinaweza kuwa tishio kubwa kwa afya yako au maisha yako ikiwa hutapata matibabu mara moja. Hii ni baadhi ya mifano, lakini dharura hazijumuishi matukio yaliyotolewa tu katika orodha hii:

- Maumivu ya kifua
- Kuvunjika mifupa
- Mpatatiko au kuanguka
- Kuvuja damu sana
- Kuchomeka sana
- Maumivu makali
- Matatizo ya afya ya akili

Huduma za baada ya dharura ili kuhakikisha kuwa afya yako ni thabiti baada ya dharura pia kushughulikiwa.

Huduma za matibabu ya dharura kama vile kushonwa, upasuaji, eksirei, au taratibu zingine, pia zinalipiwa na bima.

Ikiwa una dharura, piga simu 911 au nenda kwenye chumba cha dharura kilicho karibu au hospitali kwa huduma ya dharura papo hapo. Huhitajiki kupewa rufaa kutoka kwa PCP wako kwa huduma ya dharura. Mjulishe PCP wako kile kilichotokea haraka iwezekanavyo.

Ikiwa unahitaji huduma ya dharura wakati unasafiri nje ya mtandao wa Green Mountain Care, piga simu kwa 911 au uende kwa idara ya dharura iliyoko karibu mara moja. Green Mountain Care inawajibikia kulipia huduma ya dharura. Pia tuna jukumu la kulipia huduma zinazohitajika ili kuimarisha afya yako baada ya huduma ya dharura kutolewa.

Unapoweza kufanya hivyo, wasiliana na Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427 ili utueleze kuhusu huduma yako ya dharura. Unapaswa pia kupiga simu kwa nambari hii ukipokea bili ya huduma yako. Tutashirikiana na mtoa huduma kufuata kanuni zinazohitajika kwetu kulipia huduma yako.

Unapolazimika Kulipa

Usipofuata sheria za mpango, unaweza kulazimika kulipia huduma mwenyewe. Mifano ya wakati hali hii inaweza kutokea ni:

- Ikiwa huduma inahitaji rufaa au idhini ya awali na hujaipata kabla ya kupata kuhudumiwa;

- Ukichagua kwenda kwa mtoa huduma ambaye hakubali Green Mountain Care; na
- Ikiwa mtoa huduma wako atakuambia huduma haijalipiwa na bima, na unaamua kuipokea licha ya hilo.

Hakikisha umemwambia mtoa huduma wako kuwa unatumia Green Mountain Care. Atakuambia ikiwa hatakubali bima yako.

Fuata sheria za mpango wako ikiwa hutaki kupata bili za huduma yako ya matibabu.

Ukipokea Bili

Ikiwa unafuata sheria za mpango wako, hupaswi kupokea bili za huduma za matibabu ambazo zinaslipiwa na bima, isipokuwa kwa malipo nyongeza yoyote ambayo unaweza kuwa nayo. Ukipokea bili, fuata hatua hizi:

- Fungua bili mara moja,
- Piga simu kwa mtoa huduma na uhakikishe kuwa anajua kuwa unatumia Green Mountain Care, na
- Kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427 upate usaidizi.
- Usilipe bili kabla ya kupiga simu kwenye Kituo cha Usaidizi kwa Wateja. Green Mountain Care inaweza tu kuwalipa watoa huduma. Ukilipia huduma, hatuwezi kurejeshea pesa ulizolipa.

Ikiwa Una Bima Nyingine

Ikiwa una bima nyingine, lazima ufuate sheria za mpango wako mwingine wa bima. Nenda kwa watoa huduma ambao wako katika mpango wako wa bima na katika mipango yetu. Mtoa huduma wako lazima aitoze bima yako nyingine kwanza. Mipango yetu inaweza kusaidia kulipia kile ambacho bima yako nyingine haijalipia.

Haki na Majukumu Yako

Una haki ya

- Kutibiwa kwa heshima na uungwana,
- Kutibiwa kwa uangalifu,
- Kuchagua na kubadilisha watoa huduma wako,
- Kupata ukweli kuhusu huduma na watoa huduma wa mpango wako,
- Kupata taarifa kamili, za sasa kuhusu afya yako kuhusu masharti unayoweza kuelewa,
- Kushiriki katika maamuzi kuhusu huduma yako ya afya, ikiwemo kujibiwa maswali yako na kupata haki ya kukataa matibabu,
- Kuomba na upate nakala ya rekodi zako za matibabu unaweza kuomba mabadiliko yafanyiwe rekodi hizi ikiwa unaamini taarifa hizo si sahihi,
- Kupata maoni ya pili kutoka kwa mtoa huduma aliyehitimu ambaye ameandikishwa katika Vermont Medicaid,



Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain

Maswali: Piga simu 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898

Unaweza pia kupata huduma za wakalimani na miundo mbadala bila malipo.

- Jadili wasiwasi kuhusu mpango yako au huduma yako ya afya (angalia ukurasa wa 20 ili upate maelezo zaidi),
- Kuwa na uhuru dhidi ya aina yoyote ya vizuizi au vikwazo vinavyotumiwa kama njia ya kuendeleza uonevu, nidhamu, unyanyasaji, au ulipizaji kisasi, na
- Kuomba rufaa ikiwa umenyimwa huduma unazoamini unahitaji. Rejelea ukurasa wa 19 upate maelezo zaidi.

Una jukumu la kutunza afya yako kwa:

- Kumwambia mtoa huduma wako kuhusu dalili zako na historia ya afya;
- Kuuliza maswali unapohitaji maelezo zaidi au wakati huelewi kitu;
- Kufuatilia mipango ya matibabu ambayo wewe na mtoa huduma wako mmekubali kupokea;
- Kuweka miadi yako au kupiga simu mapema ili kughairi ikiwa huwezi kuhudhuria miadi;
- Kufahamu kuhusu sheria za mpango wako ili uweze kutumia vizuri huduma unazoweza kupata;
- Kuhakikisha una rufaa kutoka kwa PCP (inapohitajika) kabla ya kwenda kwa watoa huduma wengine;
- Kulipa marupurupu na malipo nyongeza yanapohitajika;
- Kupiga simu kughairi au kuratibu upya ikiwa huwezi kuhudhuria miadi.

Utashi wa Kuishi na Maelekezo ya Mapema

Huu hapa muhtasari wa jumla wa sheria ya Maelekezo ya Mapema ya Vermont (yanayopatikana katika Kichwa cha 18, Sura ya 231) na inamaanisha nini kwa mgonjwa:

“Maagizo ya mapema” ni rekodi iliyoandikwa ambayo inaweza kusema ni nani unachagua kutenda kwa niaba yako, ni nani mtoa huduma wako wa msingi, na maagizo yako juu ya malengo yako ya huduma ya afya au malengo ya matibabu. Inaweza kuwa mamlaka ya kudumu ya wakili kwa ajili ya huduma za afya au hati ya huduma ya mwisho. Maelekezo ya mapema hayalipishwi.

Mtu mzima anaweza kutumia maagizo ya mapema kutaja mtu mmoja au zaidi na wengine ambao wana mamlaka ya kukufanyia maamuzi ya huduma ya afya. Unaweza kuelezea kiasi cha mamlaka aliyo nayo mtu huyo, aina ya huduma ya afya unayotaka au usiyotaka, na skuema jinsi unavyotaka maswala ya kibinafsi yashughulikiwe, kama vile mipangilio ya mazishi. Maelekezo ya mapema pia yanaweza kutumika kutaja mtu mmoja au wengi wa kutumika kama mlezi ikiwa anahitajika au kutambua watu ambao hutaki wakifanya maamuzi.

Ikiwa hali yako inamaanisha kuwa huwezi kuelekeza huduma yako ya afya, na sio dharura, watoa huduma za afya hawawezi kukupa huduma ya afya bila kwanza kujaribu kujua kama una maelekezo ya mapema. Watoa huduma za afya ambao wanajua kuwa una maagizo ya mapema lazima wafuate maagizo ya mtu ambaye ana mamlaka ya kukufanyia maamuzi ya huduma za afya au kufuata maagizo yaliyo katika maelekezo ya mapema.



Mtoa huduma wa afya anaweza kukataa kufuata maagizo yaliyo katika maelekezo yako ya mapema kulingana na mgongano wa kimaadili, kidelesturi au mwingine na maagizo. Hata hivyo, ikiwa mtoa huduma wa afya atakataa, mtoa huduma lazima akuambie kuhusu mzozo, ikiwezekana, na yeyote ambaye umemtaja kuchukua hatua kwa niaba yako; kusaidia kuhamishia huduma yako kwa mtoa huduma mwingine ambaye yuko tayari kuheshimu maagizo; kutoa huduma ya afya inayoendelea hadi mtoa huduma mpya apatikane kutoa huduma; na anukuu katika rekodi yako ya matibabu mzozo huu, hatua zilizochukuliwa kutatua mzozo huu na utatuzi wa mzozo huu.

Kila mtoa huduma wa afya, kituo cha huduma za afya na kituo cha makazi kitatengeneza itifaki ili kuhakikisha kuwa maagizo yote ya mapema ya wagonjwa yanashughulikiwa kwa njia ambayo inafuata kabisa sheria na kanuni zote za serikali.

Unaweza kupiga simu kwa Idara ya Leseni na Ulinzi kwa 1-800-564-1612 au uingie mtandaoni ili kuwasilisha malalamiko kuhusu mtu ambaye hafuati sheria. Unaweza kuwasilisha malalamiko yaliyoandikwa kwa:

Ugawaji wa Leseni na Ulinzi
103 South Main Street, Ladd Hall
Waterbury, VT 05671

Unaweza kupata taarifa kuhusu sheria za serikali, maelekezo ya mapema na utashi wa maisha kwa kupiga simu kwenye Mtandao wa Maadili wa Vermont kupitia 802-828-2909 au kutembelea tovuti yao ya www.vtethicsnetwork.org.

Kichwa cha 18 kinapatikana kwenye <http://legislature.vermont.gov/statutes/chapter/18/231>. Unaweza kupata fomu unazohitaji au taarifa zaidi kwa kutembelea tovuti zilizoorodheshwa, kuzungumza na mtoa huduma wako au kukipigia simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja.

Kuchanga Viungo

Huenda ungependa kuchanga viungo vyako unapofariki. Mfadhili mmoja anaweza kuwasaidia watu wengi. Ikiwa ungependa kupata maelezo zaidi kuhusu hili, piga simu kwa 1-888-ASK-HRSA upate maelezo bila malipo.

Kushiriki Taarifa na Mtoa Huduma wako wa Msingi (PCP)

Ili kumsaidia PCP wako kuhakikisha kuwa unapata huduma ya afya unayopaswa kuwa nayo, jina lako linaweza kuwa kwenye orodha tunayompa. Baadhi ya orodha hizi zinaweza kuwa kuhusu:

- Wagonjwa wa ugonjwa wa kisukari ambao hawajapimwa macho katika mwaka mmoja uliopita,
- Wanawake ambao hawajapata kipimo cha sampuli ya tishu ya ukeni au kipimo cha mamogramu hivi karibuni,
- Watoto ambao hawajapata chanjo ya sasa,

- Dawa ambazo wagonjwa wanatumia ili kusaidia kuepuka athari mbaya za dawa ambazo hazichanganywi nazo, na
- Watoto waliochelewa katika vipimo vyako vya kawaida.

Notisi ya Kanuni za Faragha

Ulipotambuliwa kuwa unastahiki kujiunga na mipango yetu, ulipokea barua inayosema kuwa unastahiki, pamoja na nakala ya Ilani yetu ya Maadili ya Faragha. Sheria ya shirikisho, Sheria ya Bima ya Afya ya Ubebekaji na Uwajibikaji (HIPAA), inaagiza kwamba tukupe taarifa. Ilani hii inafahamisha kuhusu haki zako za faragha na kuhusu jinsi maelezo yako ya afya yanavyoweza kutumiwa au kushirikiwa. Ikiwa unahitaji nakala nyingine ya ilani, unaweza kukipigia simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja na uombe nakala. Ilani hii pia inaweza kutazamwa kwa njia ya kielektroniki kwa kutembelea www.humanservices.vermont.gov/privacy-documents.

Ikiwa unahisi kwamba haki zako za faragha zimekiukwa, tafadhali wasiliana na Afisa wa Faragha wa AHS kupitia 802-241-2234 au utembelee www.humanservices.vermont.gov/policy-legislation/hipaa/hipaa-info-beneficiaries/health-information-complaints/.

Mpango wa Uhakikisho wa Ubora

Green Mountain Care ina mpango wa uhakikisho wa ubora ili kuhakikisha kuwa unapata huduma bora za afya kutoka kwa watoa huduma wako na huduma nzuri kutoka kwa mpango wako wa afya.

Baadhi ya mambo tunayoyaangalia ili kusaidia kukadiria ubora wa huduma za afya ni:

- Wagonjwa hutumia kiasi gani cha dawa:
- Ni washiriki wangapi wanaopata huduma ya kawaida ya kinga:
- Ni washiriki wangapi wanaotumia chumba cha dharura wakati hawana dharura:
- Jinsi watoa huduma za afya ya kimwili na watoa huduma za afya ya akili wanavyoratibu huduma, na
- Jinsi washiriki na watoa huduma wanavyoridhika na mipango yetu.

Tumepitisha miongozo ya maadili bora wa kliniki kwa magonjwa fulani sugu ambayo tunawahimiza watoa huduma kufuata ili kuboresha matokeo ya afya.

Ikiwa ungependa kupendekeza njia ambazo tunaweza kutumia kuboresha mipango yetu na kufanya mipango yako ikufae zaidi, kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja. Maoni yako yatajumuishwa katika ukaguzi wetu wa uhakikisho wa ubora.

Unaweza kupata taarifa kuhusu ubora wa huduma zinazotolewa na hospitali, nyumba za uuguzi, watoa huduma za afya za nyumbani, au nakala ya miongozo ya maadili bora ya kliniki kwa kwenda kwenye www.dvha.vermont.gov/members/vermont-medicaid-programs/member-information/other-resources au kwa kupiga simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427.

Hatua ya Kuchukua Usipokubaliana na Uamuzi Tuliofanya

Unaweza kukata rufaa. Hii inamaanisha kumwomba mtu akague kesi yako na kuona ikiwa tumekosea. Endelea kusoma ili upate maelezo zaidi.

Hatua ya Kwanza ni kuamua unachokatia rufaa.

- Je, unakata rufaa kuona ikiwa unaweza kupata au kudumisha Medicaid/Dr. Dynasaur, VPharm, au Mpango wa Akiba ya Medicare? AU je, unakata rufaa ya bima?
 - Ikiwa jibu ni ndiyo, rejelea hapa chini uone kichwa cha, “Hatua ya kuchukua ikiwa hukubaliani na uamuzi wetu wa ustahiki.”
- Je, unakata rufaa ikiwa Medicaid/Dr. Dynasaur inagharimia huduma za afya?
 - Ikiwa jibu ni ndiyo, rejelea hapa chini uone kichwa cha , “Hatua ya kuchukua ikiwa hukubaliani na uamuzi kuhusu huduma zako za afya.”

Hatua ya kuchukua ikiwa hukubaliani na uamuzi wetu wa kustahiki.

Unaweza kukata rufaa kwa kuomba Usikilizaji wa Haki wa Jimbo. Afisa wa Usikilizaji katika Bodi ya Huduma za Binadamu atasikiliza kesi yako. Wataamua ikiwa Vermont Medicaid ilifanya uamuzi sahihi.

Una siku 90 za kuomba Usikilizaji wa Haki wa Jimbo. Siku 90 huanza tarehe ya kutumwa kwa taarifa ya uamuzi ambayo unakatia rufaa.

Kuna njia 3 za kuomba Usikilizaji wa Haki wa Jimbo:

- Kwa simu - - kipigie Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427;
- Mtandaoni - tembelea AHS.DVHAHealthCareAppealsTeam@vermont.gov kwenye intaneti. Ikiwa una akaunti ya mtandaoni ya VHC, unaweza kukata rufaa ndani ya akaunti yako;
- Kwa maandishi – tuma barua kwa:
 - Bodi ya Huduma za Binadamu
 - 14-16 Baldwin St., 2nd Floor
 - Montpelier, VT 05633-4301

Katika barua au barua pepe, weka jina lako, tarehe ya kuzaliwa na nambari ya simu. Sema unakata rufaa kuhusu nini na sababu yake.

Je, tulisimamisha Medicaid/Dr. Dynasaur, VPharm au Mpango wa Akiba ya Medicare? Unaweza kudumisha huduma yako ya afya wakati wa Usikilizaji wako wa Haki wa Jimbo. Tunaita hali hii “mwendelezo wa manufaa.” (Rejelea kichwa kilicho hapa chini cha, **Kuendeleza manufaa- VituMambo Mengine Unayohitaji Kujua – (Ustahiki na Huduma).**)

Lazima utume ombe hii ndani ya siku 11 baada ya notisi au kabla ya mabadiliko kuanza kutumika, chochote kitakachotokea baadaye. Siku 11 zinaanzia tarehe ambayo Vermont Medicaid ilikutumia uamuzi wake. Lazima uendelee kulipa malipo yako kwa wakati sahihi rufaa yako inapoendelea, la sivyo bima yako inaweza kuisha. Ili kuendelea kupata manufaa



VERMONT

Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain

Maswali: Piga simu 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898

Unaweza pia kupata huduma za wakalimani na miundo mbadala bila malipo.

yako ya huduma ya afya wakati wa rufaa yako, ni bora kupiga simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwenye 1-800-250-8427.

Je, unakata rufaa kuhusu malipo yako ya bima? Lazima uendelee kulipa malipo yako kwa wakati kulingana na kiasi kilichokuwa kabla ya kukutumia barua inayokufahamisha kwamba imebadilika. Usipofanya hivyo, bima yako inaweza kuisha. Tutakurudishia kiasi ulicholipa ikiwa utashinda Usikilizaji wako wa Haki wa Jimbo.

Hatua ya kuchukua unapomba Usikilizaji wa Haki wa Jimbo?

Vermont Medicaid itakagua kesi yako kabla ya kutuma ombi lako la Usikilizaji wa Haki wa Jimbo kwa Bodi ya Huduma za Binadamu. Tunaweza kuchukua hadi siku 15 ili kubaini kama tumekosea. Mwanachama wa Timu ya Rufaa ya Huduma ya Afya atawasiliana nawe ili kujadili rufaa yako. Huenda tukaweza kurekebisha tatizo lako bila kulazimika yako kwenda kwenye Usikilizaji wa Haki wa Jimbo.

Ikiwa hatuwezi kubadilisha uamuzi wetu, tutatuma ombi lako kwa Bodi ya Huduma za Binadamu. Utapata barua kutoka kwao. Afisa wa kusikiliza kesi ambaye ataamua kesi yako ataandaa mkutano ili kupata taarifa ya kuamua ikiwa Vermont Medicaid ilifanya makosa. Ni muhimu ushiriki katika mkutano huu. Unaweza kujizungumzia au kumchagua mtu azungumze kwa niaba yako.

Itachukua muda gani kufikia uamuzi? Bodi ya Huduma za Binadamu lazima iamue kesi yako ndani ya siku 90 baada ya tarehe kukata rufaa.

Je, unahitaji uamuzi wa haraka? Tuambie ikiwa kusubiri kutaathiri sana afya yako au maisha yako. Ikiwa unastahiki, Usikilizaji wa Haki wa Jimbo kwa haraka (unaoitwa “Usikilizaji wa Haki wa Jimbo kwa haraka”), uamuzi juu ya rufaa yako utafanywa haraka iwezekanavyo ikiwa utapata Medicaid kwa sababu wewe ni kipofu, mlemavu, au 65 au zaidi. Ukipata Medicaid kwa sababu nyingine, basi utapata uamuzi ndani ya siku 7.

Hatua ya kuchukua ikiwa hukubaliani na uamuzi kuhusu huduma zako za afya.

Hatua ya Kwanza ni Kuomba Rufaa ya Ndani.

Katika rufaa ya ndani, mtu katika Vermont Medicaid ambaye hakuhusika katika uamuzi wa kwanza ataangalia kesi yako na kufanya uamuzi mpya. Katika hali nyingi, lazima uwe na rufaa ya ndani kabla ya kuomba Usikilizaji wa Haki wa Jimbo.

Una siku 60 za kuomba rufaa ya ndani. Siku 60 zinaanzia tarehe ambayo Vermont Medicaid ilikutumia ilani ya uamuzi. Mtoaji huduma wako anaweza kuomba kupewa rufaa yako ikiwa unataka.

Kuna njia 3 za kuomba rufaa ya ndani:

- Nambari ya Simu: Pigia Simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwenye 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898
- Mtandaoni- tuma barua pepe kwa AHS.DVHAHealthCareAppealsTeam@vermont.gov



- Kwa barua- tuma barua kwa:

Vermont Health Connect na Green Mountain Care
Kituo cha Usaidizi kwa Wateja
101 Cherry St., Suite 320
Burlington, VT 05401

Katika barua au barua pepe, weka jina lako, tarehe ya kuzaliwa na nambari ya simu. Sema kile unachokatia rufaa, ikiwa ni pamoja na huduma ulizoomba na ikiwa ulikataliwa.

Je, tulipunguza au kusitisha huduma za afya ambazo tayari unapata? Unaweza kudumisha huduma zako wakati wa rufaa yako ya ndani. Lazima utumbe ombi hili ndani ya siku 11 au kabla ya kumalizika, chochote kitakachotokea baadaye. Siku 11 zinaanzia tarehe ambayo Vermont Medicaid ilikutumia ilani hiyo. Tunaita hali hii “mwendelezo wa manufaa.” (Rejelea kichwa kilicho hapa chini cha, **Kuendeleza manufaa- VituMambo Mengine Unayohitaji Kujua – (Ustahiki na Huduma).**)

Ili kuendelea kupata huduma zako, ni bora kupiga simu Kituo cha Usaidizi wa Huduma kwa Wateja kwenye 1-800-250-8427 ili kuomba hili.

Nini hufanyika katika rufaa ya ndani? Vermont Medicaid itaweka mkutano ili kupata taarifa ili iweze kuangalia tena uamuzi wake. Unapaswa kushiriki katika mkutano huu. Unaweza kujizungumzia au kumchagua mtu azungumze kwa niaba yako. Mtoa huduma wako anaweza kuzungumza au kutoa taarifa kwa Vermont Medicaid.

Vermont Medicaid kawaida lazima iamue rufaa yako ya ndani katika siku 30.

Inaweza kuchukua siku 14 zaidi, lakini ikiwa utafanya ombi hili au ucheleweshaji utakusaidia. (Kwa mfano, mtoa huduma wako anahitaji muda zaidi wa kutuma taarifa, au huwezi kufika kwenye mkutano au miadi katika muda ulioratibiwa awali.) Muda mrefu zaidi ambao itachukua ni siku 44 kabla ya uamuzi kufanywa.

Je, unaitaka Vermont Medicaid kuamua rufaa yako haraka? Tuambie ikiwa kusubiri kutaathiri sana afya yako au maisha yako. Ikiwa Vermont Medicaid itaamua kuwa unastahiki rufaa ya haraka (inayoitwa “rufaa iliyoharakishwa”), utapata uamuzi ndani ya saa 72. Vermont Medicaid inaweza kuchukua muda mrefu ikiwa utafanya omba hili au inaweza kukusaidia. Rufaa ya haraka zaidi inaweza kuchukua siku 17.

Una haki ya kujua jinsi tulivyoamua rufaa yako. Unaweza kuona hati, sheria na uthibitisho tuliutumia. Unaweza kuona jinsi tulivyoamua ikiwa kile ulichoomba kilikuwa muhimu kimatibabu. Unaweza kupata nakala zisizolipishwa za hati hizi zote. Ili uombe nakala, Kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427.

Je, unahitaji ushauri wa kisheria au usaidizi mwingine? Unaweza kupata usaidizi usiolipishwa kutoka kwa usaidizi wa Kisheria wa Vermont. Piga simu kwa Wakili wao wa Ofisi ya Huduma ya Afya kwa 1-800-917-7787. AU utembelee tovuti yao kwenye <https://vtlawhelp.org/> kwenye intaneti. Jaza fomu



VERMONT

Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain

Maswali: Piga simu 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898

Unaweza pia kupata huduma za wakalimani na miundo mbadala bila malipo.

Je, Unakataa Uamuzi wa Rufaa ya Ndani? Unaweza Kuomba Usikilizaji wa Haki wa Jimbo. Afisa wa Usikilizaji katika Bodi ya Huduma za Binadamu atasikiliza kesi yako. Wataamua ikiwa Vermont Medicaid ilifanya uamuzi sahihi.

Katika hali nyingi, lazima ukamilishe mchakato wa kukata rufaa wa ndani kabla ya kuomba Usikilizaji wa Haki wa Jimbo (unaoitwa “uamuzi wa mwisho”). Lakini, ikiwa Vermont Medicaid haitaamua rufaa yako ya ndani kufikia tarehe yake ya mwisho, unaweza kuomba Usikilizaji wa Haki wa Jimbo bila kusubiri uamuzi. Ikiwa tulichukua muda mrefu kuliko:

- Siku 30 kwa rufaa ya ndani AU
- Siku 44 ikiwa wewe au sisi tungeomba muda zaidi kwa sababu kuchelewa kutakusaidia
- Ikiwa ni rufaa ya haraka, saa 72 AU
- Kwa rufaa ya haraka, siku 17 ikiwa wewe au sisi tungeomba muda zaidi kwa sababu kuchelewa kutakusaidia

Una siku 120 za kuomba Usikilizaji wa Haki wa Jimbo. Siku 120 zinaanzia tarehe iliyo kwenye barua inayokufahamisha kuhusu uamuzi wa ndani wa rufaa.

Kuna njia 2 za kuomba Usikilizaji wa Haki wa Jimbo:

- Kwa simu - kipigie simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898 AU piga simu kwa Bodi ya Huduma za Binadamu kwa 802-828-2536
- Kwa barua - tuma barua kwa:

Bodi ya Huduma za Binadamu
14-16 Baldwin St., 2nd Floor
Montpelier, VT 05633-4301

Katika barua, weka jina lako, tarehe ya kuzaliwa na nambari ya simu. Sema kile unachokatia rufaa, ikiwa ni pamoja na huduma ulizoomba na ikiwa ulikataliwa.

Je, tulipunguza au kusitisha huduma za afya ambazo tayari unapata? Unaweza kudumisha huduma zako wakati wa Usikilizaji wako wa Haki wa Jimbo. LAKINI lazima uombe hili ndani ya siku 11 baada ya uamuzi wa rufaa ya ndani. Lazima uombe tena hata kama uliuliza Vermont Medicaid kuweka huduma zako sawa wakati ulisubiri rufaa yako ya ndani. Siku 11 zinaanzia tarehe ambayo Vermont Medicaid ilikutumia uamuzi wa rufaa yake. Tunaita hali hii “mwendelezo wa manufaa.” (Rejelea kichwa kilicho hapa chini cha, **Kuendeleza manufaa- VituMambo Mengine Unayohitaji Kujua – (Ustahiki na Huduma).**

Ili kuendelea kupata huduma zako, ni bora kupiga simu Kituo cha Usaidizi wa Huduma kwa Wateja kwenye 1-800-250-8427.

Hatua ya kuchukua unapoomba Usikilizaji wa Haki wa Jimbo? Utapata barua kutoka Bodi ya Huduma za Binadamu. Afisa wa kusikiliza kesi ambaye atasikiliza kesi yako ataandaa mkutano ili kupata taarifa ya kuamua ikiwa Vermont Medicaid ilifanya makosa. Ni muhimu

ushiriki. Unaweza kujizungumzia au kumchagua mtu azungumze kwa niaba yako. Mtoa huduma wako anaweza kuzungumza au kutoa taarifa afisa wa usikilizaji.

Itachukua muda gani kupata uamuzi juu ya Usikilizaji wako wa Haki wa Jimbo?

Bodi ya Huduma za Binadamu lazima iamue kesi yako ndani ya siku 90 kuanzia tarehe ulipoomba rufaa ya ndani. Hii HAIHESABU siku ulizochukua kuomba Usikilizaji wa Haki ya Serikali baada ya kupata uamuzi wa rufaa ya ndani kutoka kwa Vermont Medicaid.

Je, unahitaji uamuzi wa haraka? Tuambie ikiwa kusubiri kutaathiri sana afya yako au maisha yako. Ikiwa unastahiki kufanyiwa Usikilizaji wa Haki wa Jimbo wa haraka (unaoitwa “Usikilizaji wa Haki wa Jimbo wa haraka”), utapata uamuzi ndani ya siku 3 za kazi.

Uendelezaji wa Manufaa- Mambo Mengine Unayohitaji Kujua – (Ustahiki na Huduma)

- Ikiwa ulilipia huduma nje ya mfuko, tunaweza kuhitajika kukulipa kiasi ulicholipa ikiwa rufaa au usikilizaji umeamuliwa kwa niaba yako.
- Iwapo tulilipia manufaa yanayoendelea na ukapoteza rufaa yako, **unaweza kulazimika** kulipa gharama ya manufaa yoyote uliyopata wakati rufaa ilikuwa inasubiri.
- Unaweza kuomba manufaa yanayoendelea unapoomba rufaa ya ndani au Usikilizaji wa Haki wa Jimbo.
- Huduma au manufaa ya afya hayawezi kuendelea ikiwa rufaa yako ya ndani au Usikilizaji wa Haki wa Jimbo unahusu manufaa ya huduma au huduma ya afya ambayo yamemalizika au kupunguzwa kwa sababu ya mabadiliko ya sheria ya shirikisho au serikali.

Je, unahitaji ushauri wa kisheria au usaidizi mwingine kuhusu rufaa yako?

Unaweza kupata usaidizi usiolipishwa kutoka kwa usaidizi wa Kisheria wa Vermont. Piga simu kwa Wakili wao wa Ofisi ya Huduma ya Afya kwa **1-800-917-7787**. AU utembelee tovuti yao kwenye <https://vtlawhelp.org/> on the internet. Jaza fomu.

Aina nyingine za malalamiko kuhusu huduma zako za afya – unaweza kuwasilisha Nung’uniko

Nung’uniko ni malalamiko kuhusu mambo ambayo hayawezi kukatiwa rufaa, kama vile eneo au urahisi wa kumtembelea mtoa huduma wako wa afya, ubora wa huduma za afya zinazotolewa, au kuathiriwa baada ya kutumia haki zako. Unaweza kuwasilisha nung’uniko wakati wowote. Unaweza kuwasilisha nung’uniko kwa kukipigia simu Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427

Itakuwaje ikiwa hujaridhika na jinsi nung’uniko lako lilivyoshughulikiwa? Unaweza kuomba Tathmini ya Nung’uniko. Mtu asiyeegemea upande wowote atakagua Nung’uniko lako ili kuhakikisha kuwa mchakato wa Nung’uniko ulishughulikiwa kwa haki. Utapokea barua yenye matokeo ya tathmini.



VERMONT

Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain

Maswali: Piga simu 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898

Unaweza pia kupata huduma za wakalimani na miundo mbadala bila malipo.

Unahitaji Usaidizi?

Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain
Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain kipo ili kukusaidia. Wanaweza kujibu maswali kuhusu mpango wako, kukusaidia kuchagua au kubadilisha PCP wako, na kukusaidia ikiwa unatatizika kupata huduma za afya.

Wafanyakazi wa Kituo cha Usaidizi kwa Wateja wanapatikana kuanzia 8:00 a.m. hadi 4:30 p.m., Jumatatu hadi Ijumaa (likizo zilizofungwa) kwa 1-800-250-8427 au TDD 1-888-834-7898.

Ripoti mabadiliko ndani ya siku 10 baada ya mabadiliko:

- Mabadiliko ya mapato yako au familia;
- Mabadiliko ya anwani;
- Kuzaliwa au kuasili watoto;
- Vifo; na
- Bima nyingine ya afya unayopata.

Ofisi ya Wakili wa Huduma ya Afya (HCA)

Ofisi ya Wakili wa Huduma ya Afya inapatikana ili kukusaidia ukiwa na matatizo ya huduma yako ya afya au manufaa yako. Ofisi ya Wakili wa Huduma ya Afya inaweza pia kukusaidia kwa malalamiko, rufaa, na usikilizaji wa haki. Unaweza kupiga simu kwa ofisi ya HCA kwa 1-800-917-7787.

Maelezo ya Ziada

Tunafurahi kutoa taarifa kwa wanachama kuhusu mipango, huduma na watoa huduma wetu. Mbali na maudhui yaliyo katika mwongozo huu, unaweza pia kuwasiliana na Kituo cha Usaidizi kwa Wateja kwa 1-800-250-8427 au utembelee www.dvha.vermont.gov upate maelezo au ulize maswali ya ziada.

Mipango Mwingine

Kuna mpango na huduma nyingine zinazopatikana kwa watoto, watu wazima na familia. Usafiri wa kwenda huduma hizi unaweza kupatikana kulingana na mpango wako uliojiandikisha. Ili upate maelezo zaidi kuhusu ustahiki wa usafiri, piga simu kwenye Kituo cha Usaidizi kwa Wateja. Baadhi ya mipango hii ina masharti ya ziada ya ustahiki. Ikiwa una maswali au unataka kufahamu ikiwa unastahiki, piga simu kwa nambari ya mpango mahususi iliyoorodheshwa hapa chini.

Huduma za Utunzaji wa Watu Wazima

Huduma za Utunzaji wa Watu Wazima hutoa huduma mbalimbali ili kuwasaidia watu wazima wa kawaida na watu wazima wenye ulemavu kuendelea kujitegemea kadri iwezekanavyo katika nyumba zao wenyewe. Huduma za Utunzaji wa Watu Wazima hutolewa katika vituo vya mchana vya jamii, visivyo vya makazi vinavyotoa mazingira salama, ya

kuunga mkono ambapo watu wanaweza kupata huduma za afya na za kijamii. Ili upate maelezo zaidi, piga simu kwa Idara ya Ulemavu, Uzee na Maisha ya Kujitegemea (DAIL) kwenye (802) 241-2401 au utembelee <https://asd.vermont.gov/services/adult-day-services>.

Mpango wa Huduma za Wasaidizi

Mpango huu unasaidia maisha ya kujitegemea kwa watu wazima wenye ulemavu ambao wanahitaji usaidizi wa kimwili katika shughuli za kila siku. Washiriki wa mpango huajiri, kufundisha, kusimamia na kupanga (mhudumu) wahudumu wao binafsi. Kwa maelezo zaidi, piga simu kwa Idara ya Ulemavu, Wazee <https://asd.vermont.gov/services/attendant-services-program> na Kuishi kwa Kujitegemea (DAIL) kwenye (802)-241-2401 au utembelee <https://asd.vermont.gov/services/attendant-services-program>.

Huduma Jumuishi za Watoto (CIS)

CIS ni rasilimali ya wanawake wajawazito au baada ya kujifungua na familia zilizo na watoto wa umri wa kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka sita. Timu zina utaalum katika kazi za kijamii na usaidizi wa familia; afya ya mama/mtoto na uuguzi; ukuaji wa mtoto na uingiliaji kati wa mapema; afya ya kiakili ya utotoni na familia; utunzaji wa mtoto; na utaalum mwingine (kwa mfano, lishe, usemi na tiba ya lugha). Ili upate maelezo zaidi, wasiliana na Idara ya Maendeleo ya Watoto na Familia kupitia (802) 241-3110 au 1-800-649-2642 au tembelea <https://dcf.vermont.gov/services/cis>

Huduma Jumuishi za Watoto - Uingiliaji Kati wa Mapema (CIS-EI)

Huu ni mpango maalum kwa watoto wa umri wa chini ya miaka 3 ambao wana ulemavu au ucheleweshaji wa kukua. Hutoa huduma za uingiliaji kati wa mapema kwa watoto wachanga, watoto wakubwa na familia. Ili upate maelezo zaidi, piga simu kwa Vermont Family Network kupitia 1- 800- 800- 4005.

Huduma za Utunzaji Binafsi wa Watoto

Huduma za Utunzaji wa Kibinafsi wa Watoto ni huduma ya moja kwa moja wa Watoto wenye Mahitaji Maalum ya Afya (CSHN) – ni huduma ya Medicaid inayopatikana kwa watu walio chini ya umri wa miaka 21 ambao wana ulemavu mkubwa, wa muda mrefu au hali ya kiafya ambayo inaathiri sana maendeleo yao yanayofaa umri na uwezo wa kufanya shughuli za maisha ya kila siku (ADL). Lengo la Huduma za Utunzaji wa Kibinafsi wa Watoto (CPCS) ni kutoa usaidizi wa ziada na utunzaji wa kibinafsi kwa mtoto. Kwa taarifa zaidi, piga simu 1-(800)-660-4427 au (802)-863-7338 au utembelee <https://www.healthvermont.gov/children-youth-families/children-special-health-needs/personal-care-services>.

Kliniki za Watoto wenye Mahitaji Maalum ya Kiafya (CSHN)

Mpango huu hutoa kliniki na huduma za uratibu wa huduma kwa watoto wenye mahitaji maalum ya afya. Pia husaidia katika baadhi ya gharama za huduma za afya ambazo hazijashughulikiwa na bima ya afya au ya Dr. Dynasaur. Piga simu kwa Idara ya Afya ya Vermont kwa 1-(800) -660-4427 au (802)-863-7338 au utembelee <https://www.healthvermont.gov/family/special-health-needs>.

Machaguo ya Utunzaji

Machaguo ya Utunzaji ni mpango wa utunzaji wa muda mrefu wa kulipia utunzaji na usaidizi kwa WanaVermont wazee na watu wenye ulemavu wa kimwili. Mpango huu huwasaidia watu kufanya shughuli za kila siku nyumbani, katika mazingira bora ya utunzaji unaotolewa katika

makazi, au katika kituo cha uuguzi. Watoa huduma ni Vituo vya Mchana vya Watu Wazima, Wakala wa Vituo vya Wazee na Usaidizi wa Maisha, Wakala wa Afya ya Nyumbani, Vituo vya Uuguzi, na Vituo vya Utunzaji Unaotolewa Nyumbani. Ili upate maelezo zaidi, piga simu (802) 241-0294 au utembelee <https://asd.vermont.gov/services/choices-for-care-program>.

Huduma za Ulemavu wa Kiukuaji

Huduma za ulemavu wa maendeleo husaidia kuwadumisha watu wa umri wowote ambao wana ulemavu wa ukuaji wanaoishi nyumbani na familia zao. Huduma hizi ni pamoja na usimamizi wa kesi, huduma za ajira, usaidizi wa jamii, na huduma za kupumzika. Watoa huduma lazima wawe watoa huduma za ukuaji au Mashirika ya Huduma za Upatanishi kwa watu wanaojisimamia wenyewe. Ili upate maelezo zaidi, piga simu kwa Idara ya Watu wenye Ulemavu, Wazee na Wanaoishi kwa Kujitegemea (DAIL) kwenye (802) 241-0304 au utembelee <https://ddsd.vermont.gov/>.

Mpango wa Usaidizi wa Kifedha

Mpango wa hiari ambao unaweza kusaidia familia kulipia gharama za baada ya bima ya huduma ya afya ya mtoto wao wakati huduma zimeagizwa au kuidhinishwa mapema kupitia mpango wa kliniki wa CSHN. Piga simu kwa Idara ya Afya ya Vermont kwa 1-(800) -660-4427 au (802)-863-7338 au utembelee <https://www.healthvermont.gov/children-youth-families/children-special-health-needs/care-coordination>.

Ufadhili Rahisi wa Familia

Ufadhili Rahisi wa Familia ni wa watu wa umri wowote ambao wana ulemavu wa ukuaji na wanaoishi na familia, au kwa familia ambazo zinaishi na kumsaidia mwanafamilia mwenye ulemavu wa ukuaji. Mpango huo unakubali kwamba familia kama walezi hutoa makazi ya asili na ya kuwezesha ukuaji zaidi kwa watoto na watu wazima wengi wenye ulemavu wa ukuaji. Fedha zinazotolewa zinaweza kutumiwa kwa uamuzi wa familia kwa huduma na misaada ili kumfaidi mtu binafsi na familia. Watoa huduma ni watoa huduma za ukuaji (Mawakala Walioteuliwa). Ili upate maelezo zaidi, ipigie simu Idara ya Huduma za Maendeleo ya Ulemavu, Wazee na Kuishi kwa Kujitegemea (DAIL) kwa (802) 241-0304 au utembelee <https://ddsd.vermont.gov/flexible-family-funding>.

Huduma ya Uuguzi Unaotumia Teknolojia ya Hali ya Juu

Mpango wa Huduma ya Uuguzi Unaotumia Teknolojia ya Hali ya Juu ni mpango wa kina wa uuguzi wa nyumbani kwa watu ambao wanategemea teknolojia kuishi au wenye mahitaji tata ya kimatibabu. Malengo yake ni kuwezesha mpito kutoka hospitalini au huduma nyingine ya kitaasisi kwenda nyumbani na kuzuia kupelekwa katika taasisi. Ili upate maelezo zaidi kwa watu wenye umri wa zaidi ya miaka 21, piga simu kwa Idara ya Watu wenye Ulemavu, Wazee na Wanaoishi kwa Kujitegemea (DAIL) kupitia (802) 241-0294 au utembelee <https://asd.vermont.gov/services/adult-high-technology-services>.

Mpango wa Uuguzi wa Nyumbani Unaotumia Teknolojia ya Hali Juu kwa Watoto unasimamiwa na Watoto wenye Mahitaji Maalum ya Afya kwa watu walio chini ya umri wa miaka 21. Ili upate maelezo, piga simu kwa 1-(800) -660-4427 au (802)-863-7338 au utembelee <https://www.healthvermont.gov/children-youth-families/children-special-health-needs/high-tech-nursing>.

Huduma za Utunzaji wa Nyumbani

Mpango wa Utunzaji wa Nyumbani wa Vermont huwasaidia watu wa umri wa miaka 18 na zaidi wenye ulemavu ambao wanahitaji usaidizi wa mahitaji binafsi au kazi za nyumbani kuishi nyumbani. Huduma hizi ni pamoja na kununua bidhaa, kusafisha nyumbani na kufua nguo. Huduma hizi huwasaidia watu kuishi nyumbani kwa kujitegemea katika mazingira yenye afya na salama. Watoa huduma ni Mashirika ya Afya ya Nyumbani. Ili upate maelezo zaidi, piga simu kwa Idara ya Watu wenye Ulemavu, Wazee na Wanaoishi kwa Kujitegemea (DAIL) kwenye (802) 241-0294 au utembelee <https://asd.vermont.gov/tags/homemaker>.

Kliniki Maalum

Hizi ni kliniki za tasnia anuwai, za watoto, zinazosimamiwa au kuimarishwa na wauguzi na wahudumu wa kijamii wa matibabu, na kuunda mfumo kamili, unaozingatia familia, ulioratibiwa na wenye huduma za moja kwa moja. Kliniki hizi zimeboba katika Tiba ya Moyo; Ukuaji wa Watoto; Upasuaji wa Midomo na Fizi; Uvimbe Mdogo; Kifafa/Tiba ya Neva; Jongu ya Mikono au Mifupa kwa Watoto; Umeng'enyaji; Kufura kwa Uti wa Mgongo; Uharibifu wa Misuli; Mifupa; Upasuaji wa Neva na hali zinginezo. Piga simu kwa Idara ya Afya ya Vermont kwa 1-(800) 464-4343 au (802)-863-7200 au utembelee <https://www.healthvermont.gov>

Huduma Maalum

Wauguzi wa CSHN au wahudumu wa kijamii wa matibabu ambao wako katika ofisi za wilaya za Idara ya Afya za mkoa hutoa usaidizi wa upatikanaji na uratibu wa huduma maalum za afya ambazo hazipatikani kupitia kliniki za huduma za moja kwa moja za CSHN. Piga simu kwa Idara ya Afya ya Vermont kwa 1-(800) 464-4343 au (802)-863-7200 au utembelee www.healthvermont.gov.

Mpango wa Vermont wa Kugundua na Kutibu Mapema Matatizo ya Masikio

Mpango wa Vermont wa Kugundua na Kutibu Mapema Matatizo ya Masikio (VTEHDI) hutoa usaidizi, mafunzo na usimamizi wa utunzaji kwa familia na watoto wao, na kwa watoa huduma wa jamii. Ushirikiano huu husaidia kwa mialiko ya wakati unaofaa kwa ajili ya vipimo vya uchunguzi na huduma za matibabu ya mapema. Ili upate maelezo zaidi kuhusu mpango wowote kati ya hii, tafadhali piga simu kwa 1-(800) 537-0076 au (802)-651-1872 au utembelee <https://www.healthvermont.gov/family/health-care/hearing-health>.

Afya ya Akili

Jimbo la Vermont linawapa kandarasi wakala walioteuliwa nchini kote kutoa huduma mbalimbali za afya ya akili kwa watu binafsi na familia zinazokabiliwa na dhiki kubwa ya kihisia, ugonjwa wa akili, au matatizo ya kitabia yenye ukali wa kutatiza maisha yao. Huduma zinatofautiana kutoka wakala mmoja hadi mwingine, lakini mipango ya msingi inapatikana katika wakala wote walioteuliwa. Waratibu wa usajili katika kila kituo hushirikiana na watu binafsi ili kuamua mipango na huduma zinazopatikana ili kukidhi mahitaji ya mtu binafsi. Aidha, mawakala walioteuliwa hutoa ufikiaji kama inavyohitajika kwa huduma kadhaa za jimbo zima kwa ajili ya utunzaji wa kina unatolewa katika makazi, vitanda vya dharura au vya rufaa ya hospitalini, na utunzaji wa wagonjwa wa hospitalini. Ili kuwasiliana na Idara ya Afya ya Akili, piga simu (802) 241-0090 au utembelee <https://mentalhealth.vermont.gov/>.



VERMONT

Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain

Maswali: Piga simu 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898

Unaweza pia kupata huduma za wakalimani na miundo mbadala bila malipo.

Huduma za Watu Wazima Wasioishi Kituoni

Mpango huu hutoa huduma ambazo hutofautiana kutoka kwa wakala mmoja hadi mwingine, na orodha za kusubiri ni za kawaida. Huduma zinaweza kujumuisha tathmini, ushauri nasaha, maagizo ya dawa na ufuatiliaji, pamoja na huduma kwa watu wa umri wa miaka sitini na zaidi wenye mahitaji ya huduma ya afya ya akili. Baadhi ya huduma zinapatikana kupitia watoa huduma binafsi, na baadhi ya watu wanaweza kutumwa kwao.

Huduma kwa Watoto, Vijana na Familia

Mpango huu hutoa huduma na usaidizi wa matibabu kwa familia ili watoto na vijana walio na matatizo ya afya ya akili waweze kuishi, kujifunza, na kukua wakiwa na afya katika shule na jamii yao. Huduma hizi ni pamoja na uchunguzi, huduma za kuzuia, usaidizi wa kijamii, matibabu, ushauri nasaha, na kukabiliana na matatizo.

Urekebishaji na Matibabu ya Kijamii

Mpango huu hutoa huduma za afya ya akili za jamii ili kuwezesha watu kuishi kwa kujitegemea kwa hali ya juu katika jamii zao kati ya familia, marafiki na majirani. Huduma kamili za CRT zinapatikana tu kwa watu wazima walio na ugonjwa mkali na unaoendelea wa akili na utambuzi unaostahiki ambao unakidhi vigezo vya ziada vya kustahiki ikiwa ni pamoja na utumiaji wa huduma na historia ya kulazwa hospitalini, kiwango cha ulemavu, na ulemavu wa kiutendaji.

Huduma za Dharura

Mpango huu hutoa huduma za dharura za afya ya akili saa ishirini na nne kwa siku, siku saba kwa wiki kwa watu binafsi, mashirika na jamii. Huduma muhimu za dharura zinaweza kujumuisha usaidizi wa njia ya simu, tathmini ya ana kwa ana, rufaa na mashauriano.

Mpango wa Majeraha ya Ubongo

Mpango huu huwasaidia WanaVermont wa umri wa miaka 16 au zaidi waliogunduliwa na jeraha la wastani hadi kali la ubongo. Mpango huu huwachukua au kuwarudisha watu kutoka hospitalini hadi vituo vyenye mazingira ya kijamii. Huu ni mpango unaotumia urekebishaji, unaoendeshwa kulingana na machaguo na unaokusudiwa kuwasaidia watu kufikia kiwango cha juu zaidi cha kujitegemea na kuwasaidia kurudi kazini. Ili upate maelezo zaidi, piga simu kwa Idara ya Watu wenye Ulemavu, Wazee na Wanaoishi kwa Kujitegemea (DAIL) kwenye (802) 241-0294 au utembelee <https://asd.vermont.gov/services/tbi-program>.

Mpango kwa Wanawake, Watoto Wachanga na Watoto Wakubwa (WIC)

WIC ni mpango wa lishe ambao hutoa vyakula bora, elimu ya lishe, usaidizi wa kunyonyesha kwa kina mama wajawazito, au waliojifungua, na watoto wachanga na watoto wakubwa wa umri wa hadi miaka 5. Mtu yeyote katika Medicaid anastahiki kushiriki katika mpango wa WIC. Ili upate maelezo zaidi na utume ombi la WIC mtandaoni, tembelea www.healthvermont.gov/family/wic au utume ujumbe unaosema VTWIC kwa 855-11.

Maelezo zaidi kuhusu nyenzo katika jumuiya yako yanaweza kupatikana katika www.vermont211.org.

Makinika! Ikiwa unahitaji usaidizi katika lugha yako, tafadhali piga simu kwa 1-800-250-8427

انتباه! إذا كنت بحاجة إلى مساعدة بلغتك ، فيرجى الاتصال على 1-800-250-8427

Pažnja! Ako vam je potrebna pomoć na vašem jeziku, pozovite 1-800-250-8427

သတိပြုရန်! မိတ်ဆွေသည် သင့်ဘာသာစကားဖြင့် အကူအညီ လိုပါက၊
ကျေးဇူးပြုပြီး 1-800-250-8427 ကိုခေါ်ပါ။

توجه! اگر شما نیاز به کمک در زبان خود، لطفاً با شماره تلفن 1-800-250-8427

Attention! Si vous avez besoin d'assistance dans votre langue, appelez le 1-800-250-8427

Nurabe maso! Niba ukeneye ubufasha mu rurimi rwawe, wahamagara kuri 1-800-250-8427

ध्यान! यदि तपाईंलाई आफ्नो भाषामा मद्दत चाहिन्छ भने, कृपया 1-800-250-8427 मा कल गर्नुहोस्

پاملرنه! که تاسو په خپله ژبه کې مرستې ته اړتیا لرئ، مهرباني وکړئ 1-800-250-8427 ته زنگ ووهئ

Ogow! Haddii aad u baahan tahay in lagugu caawiyo luqaddada, fadlan wac 1-800-250-8427

¡Atención! Si necesita ayuda en su idioma, por favor llame al 1-800-250-8427

Muhimu! Kama wahitaji usaidizi kwa lugha yako, tafadhali piga simu 1-800-250-8427

Uvaha! Yakshcho vam potribna dopomoha vashoyu movoyu, telefonuyte za nomerom 1-800-250-8427



Kituo cha Usaidizi cha Vermont Health Connect na Green Mountain

Maswali: Piga simu 1-800-250-8427 (TDD/TTY) 1-888-834-7898

Unaweza pia kupata huduma za wakalimani na miundo mbadala bila malipo.